



# Kibali cha kusafiri nje ya Nchi kwa Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai

## Nifuate hatua zipi ili nipate kibali?

### 1. SAJILIWA KWENYE MFUMO NA AFISA TEHAMA

Mwombaji hakikisha una taarifa zifuatazo

- Majina yako matatu
- Namba yako ya simu
- Barua pepe yako
- Idara/kitengo unakotoka Mfano TEHAMA/ELIMU SEKONDARI N.K
- Cheo chako Mfano Information Communication Technology Officer (ICTO)



### 2. HUISHA AKAUNTI YAKO YA MFUMO WA KUOMBA KIBALI

- Ingia kwenye anuani ya barua pepe yako(uliyosajiliwa nayo), utakuta barua pepe
- Fuata maelekezo uliyopewa kwenye barua pepe yako ili kuweka nenosiri/nywila (password) mpya.
- Kuingia kwenye mfumo tumia <https://www.safari.gov.tz> kisha andika anuani ya barua pepe yako pamoja na neno siri/nywila uliyotengeneza.

### 3. JINSI YA KUOMBA KIBALI

Mmwombaji awe na taarifa/nyaraka zifuatazo (Nyarakka zote ziwe fomati ya pdf)

- Namba ya hati ya kusafiria (passport number)
- Tarehe ya safari (Iwe siku 21 au zaidi kabla ya tarehe/siku ya safari).
- Kiasi cha nauli na posho unayotakiwa kulipwa/kupewa (Kama safari inagharamiwa na Serikali)
- Barua ya mwaliko kutoka nchi utakayoenda
- Barua ya utambulisho kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (Mkuu wa Taasisi)
- Fomu ya likizo kama safari ni binafsi mfano mapumziko/matembezi n.k
- Fomu ya rufaa ya matibabu (Safari kwa ajili ya matibabu)
- Barua ya udahili, mdhamini na mwaliko (Safari ya kimasomo ya muda mrefu)

NB: Afisa TEHAMA atakupa maelekezo ya kuomba kibali kwenye mfumo mara tu nyarakka zote zitakapokamilisha na kuwasilisha kwa kuzingatia vigezo vilivyokubalika.

#### 4. JINSI YA KUFUATILIA KIBALI

Mara baada ya kujaza fomu kwenye mfumo na kubonyeza neno **WASILISHA**, Maombi yako yatafika kwa **Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Hai(Mkuu wa taasisi)**. Mtaarifu ili aidhinishe kibali chako kiweze kwenda hatua inayofuata.

- Hatua/hali za maombi ya kibali chako yataonekana kwenye mfumo kupitia akauti yako ya mfumo au
- Unaweza kufuutilia maombi kwa njia ya simu,  
Andika neno KIBALI acha nafasi ikifuatiwa na Namba ya kumbukumbu (Mfn: KIBALI V12345678) halafu tuma kwenda 15200. Ujumbe mmoja utakugharimu Tsh. 100 tu.

#### Nitakiona vipi kibali?

- Ingia kwenye akauti yako ya mfumo kisha bonyeza kiungio “*Maombi yalyoidhinishwa*”
- Bonyeza kiungio (link) iliyoandikwa “View” upande wa kulia
- Kibali kitafunguka na unatakiwa kuchapisha (print) ukiwa ndani ya mfumo *Maombi yalyoidhinishwa (1)*

#	Tarehe ya Kuomba	Jina	Taasisi	Nchi Unayoenda	Tarehe ya Safari	Aina ya Kibali	Hali	Hatua
1	22-11-2018		HAI DISTRICT COUNCIL	Morocco	04-12-2018	Dharura	Yalyoidhinishwa	 

Imeandaliwa na Anold T Malisa, afisa TEHAMA

ICT for Service Delivery and Development  
TEHAMA kwa Utoaji wa Huduma na Maendeleo